# JINSI YA KUONGEZA THAMANI YAKO

**Njia Za Uhakika Zitakazokufanya Ulipwe Mpaka Mara Kumi Zaidi Ya Unavyolipwa Sasa.**


**GODIUS RWEYONGEZA**

**www.songambele.co.tz**

# UTANGULIZI

Rafiki yangu mpendwa

Salaam,

Moja ya kitu muhimu sana unachopaswa kukifanyia kazi kwenye maisha yako ni thamani yako. Ila kwanza labda tujiulize thamani ni nini? Ili tujue maana halisi ya thamani nimelazimika kuangalia kwenye kamusi ya Kiswahili sanifu, ambayo inasema Kuwa **thamani ni gharama au ubora wa kitu kutokana na hali na kuhitajika kwake na jamii**.

Sawa hiyo ni maana ya thamani, na je, ipi itakuwa maana ya thamani binafsi. Thamani yako tunaweza kuiona kwa kuangalia vitu viwili **muda** na **kiasi cha pesa** unacholipwa ndani ya huo muda. Kwa mfano, kuna mtu kwa siku anaingiza kipato cha milioni kumi. Wakati kuna ambaye anaingiza kipato cha laki moja. Na wakati huohuo kuna ambaye hata elfu kumi hapati.

Kumbe hawa watu watatu **thamani yao binafsi** haiwezi kuwa moja. Pengine unajiuliza, imekuwaje mimi nimeamua thamani ya mtu ipimwe kwa kiwango cha fedha anachoingiza. Ukweli ni kuwa siyo mimi niliyegundua hili. Hiki ni kitu ambacho watu wengi wamekuwa wanakitumia kutoa thamani kwa watu, na hata kwenye familia nyingi mtu mwenye pesa anathaminiwa sana kuliko ambaye hana fedha.

Vikiitishwa vikao vya familia, kama kuna kuna watu wawili, mmoja mlevi mlevi na mwingine ni mtu ambaye anafanya biashara na ana kipato kizuri. Ikitokea mlevi akachangia kitu, watu watasema huo ni ulevi hata kama kaongea pointi ya maana, ila mwenye hela hata akiongea pumba, anaonekana ameongea pointi na hata kupigiwa makofi. Chezea hela wewe! Mtu mwenye hela yake anaitwa *bosi mkubwa* hata kama ni mdogo. Hahaha.

Sasa kwa kwa vile tunaishi kwenye dunia ambayo inathamanisha watu hivyo, hatuna budi kujua hili ili tuongeze thamani zetu au wewe unasemaje? Wewe pia unapaswa kujua thamani yako kwa sasa hivi, lakini pia unapaswa kufanya juhudi ili kufanya thamani yako iongezeke zaidi.

Mbinu unazoenda kujifunza kwenye kitabu hiki zitakusaidia kuongeza thamani yako mara mbili mpaka mara kumi zaidi. Yaani, utaweza kulipwa mara mbili mpaka mara kumi zaidi ya unavyolipwa sasa hivi. Kumbe basi naomba nieleweke kwenye suala moja tu, ninaposema kwamba unaenda kujifunza mbinu za kukusaidia wewe kuongeza thamani yako. Simaanishi kwamba, utaongeza thamani kwa kuwa mrembo zaidi. Wala simaanishi kwamba utaongeza thamani kwa kupata *followers* zaidi mtandaoni, na wala simaanishi kwamba unaongeza thamani yako kwa kuwa mrefu, mfupi, mtu wa miraba minne, mweusi, mweupe au maji ya kunde!

Bali namaanisha kuongeza thamani kwa kulipwa zaidi. Ukitumia mbinu zilizoainishwa kwenye hiki kitabu, utakuwa na uwezo wa

kulipwa mara mbili mpaka mara kumi zaidi. Hivi kwa mfano unaanzaje kuacha kutumia mbinu hizi ili uweze kulipwa zaidi ya unavyolipwa sasa hivi.

Kabla hatujazama zaidi kwenye kitabu, ngoja kwanza tuone namna unavyoweza kujua thamani ya muda wako kwa sasa

**Jinsi Ya Kujua Thamani Ya Muda Wako**

Mimi na wewe tuna bahati ya kuwa na rasilimali nyingi ambazo tunaweza kutumia kwenye maisha yetu ya kila siku.

Rasilimali hizo ni kama

- Ardhi
- Madini
- Maji
- Fedha
- Muda ……

Kati ya hizo rasilimali zote, muda ndio rasilimali ambayo ukiipoteza huwezi kuipata. Hivyo, unahitaji kuweza kuitumia vizuri rasilimali hii ya kipekee.

Na leo nataka nikwambie namna ambavyo unaweza kujua thamani ya muda wako. Kujua thamani kutakusaidia zaidi kuwekeza nguvu zako kwenye kufanya kazi na majukumu ambayo ni ya muhimu, huku ukiachana na majukumu ambayo siyo ya muhimu

Ili tujue thamani ya muda wako, kwanza unapaswa kujua kiasi gani unataka kuingiza kwa mwaka mmoja ujao. Ebu kwa mfano tuseme kwamba una mpango wa kuingiza milionoi 100. (Hiki kitu tukiite A)

Kitu cha pili cha kujiuliza ni muda kiasi gani ambao uko tayari kufanya kazi kwa wiki? Kama kwa siku unafanya kazi kwa saa 15 na kwa wiki unafanya kazi kwa siku sita. Maana yake kwa wiki unafanya kazi kwa saa 90 (Hiki kitu tukiite B).

Na kitu cha tatu ambacho tunataka tujue ni je, kwa mwaka utakuwa tayari kufanya kazi kwa wiki ngapi? Kwa kawaida mwaka una wiki 52. Sasa ni wiki ngapi utakuwa tayari kufanya kazi ukiondoa wiki za mapumziko. Kama unapumzika kwa mwezi mzima kwa mwaka, maana yake unafanya kazi kwa wiki 48 tu kwa mwaka (hiki kitu tukiite C).

Sasa kifuatacho, ngoja tuone thamani ya muda wako kwa kutumia vipengele hivyo hapo juu. Kujua thamani ya muda wako utachukua.

Thamani ya saa lako moja= (A÷B÷C)

Kwa hiyo kama una mpango wa kuingiza milioni 100 (100,000,000) kwa mwaka na upo tayari kufanya kazi kwa saa 90 kwa wiki kwa wiki 48. Hivyo,

Thamani ya saa lako moja=(100,000,000÷90÷48)=23,146

Kwa hiyo wewe thamani ya saa moja kwako ni sawa na 23,148. Ukifanya kazi yoyote ambayo ni ya chini ya hivyo viwango, basi unakuwa umejishusha.

Kama ulikuwa hujawahi kupima thamani ya muda wako, Ebu fanya hivyo siku ya leo. Utajifunza vitu vingi na kikubwa zaidi ni kwenye utunzaji mzuri wa muda wako ili kazi unazofanyaa ziendane na viwango vya thamani yako.

Lakini ubora ni kwamba unaweza kuongeza thamani ya saa lako moja kutoka kiwango cha chini na kukipandisha juu kabisa.

Hakuna kiwango cha ukomo wa thamani ya muda wako unachoweza kutengeneza

Sasa wacha tuzame ndani zaidi kwenye hiki kitabu ili uweze kuona ni kwa namna gani unaweza kuongeza thamani yako hatua kwa hatua. Mbinu unazoenda kujifunza kwenye hiki kitabu ni mbinu ambazo wanatumia watu wanaolipwa kiwango kikubwa cha fedha kwa siku, wiki na mwezi. Ubora ni kuwa mbinu hizi ukizitumia wewe mwenyewe unaenda kupata matokeo makubwa ambayo hata hapo awali ulikuwa hujafikiria kuwa unaweza kuyapata.

Miaka kadhaa iliyopita nilikuwa namsikiliza Les Brown, kwenye yale maongezi akawa anasema kwamba alipokuwa anaitwa kwenye semina alikuwa analipwa dola elfu moja kwa kila maongezi. Ila sasa siku moja katika kuongea na baadhi ya watu waliokuwa wanatengeneza kiasi kikubwa zaidi ya hapo, walimwambia kuwa unaweza kulipwa zaidi ya

hapo. Wakamwambia kuwa badala ya kulipwa dola elfu moja unaweza kulipwa mpaka dola elfu tano kwa saa moja. Les Brwon anasema kwamba hiki kitu kilimpa hofu kwanza, lakini baadaye alipoanza kukifanyia kazi, kitu hiki kikaleta matokeo makubwa akawa ameanza kulipwa hicho kiasi na baadaye akaweza kulipwa zaidi ya hapo.

Ninachotaka kukwambia ni kuwa, unaweza kulipwa zaidi ya unavyolipwa sasa hivi. na mbinu zilizoainishwa kwenye hiki kitabu zinajieleza waziwazi tu.

Wasalaam,

Godius Rweyongeza
0755848391
Morogoro-Tz
24 Agosti, 2022.

# YALIYOMO

UTANGULIZI........................................................................2

SURA YA KWANZA ................................................................13

KUWA NA KITU AMBACHO HAKUNA MTU ANAWEZA KUKIFANYA ..........................................................................13

SURA YA PILI ......................................................................20

ACHA MAZOEA na FANYA KAZI ZAIDI YA UNAVYOLIPWA .....20

Huu Ndio Ulevi Pekee Ambao Unapaswa Kuwa Nao ..........28

SURA YA TATU ....................................................................34

AINA TATU ZA UJUZI UNAOHITAJI ILI KUONGEZA THAMANI YAKO NA KULA MEMA YA NCHI ...........................................34

SURA YA NNE......................................................................50

NGUVU YA KUFANYA MAZOEZI ..................................50

SURA YA TANO ...................................................................67

NGUVU YA SAA ELFU KUMI ..................................................67

SURA YA SITA......................................................................71

JINSI UBUNIFU UNAVYOWEZA KUKUINUA KWENYE BIASHARA .......................................................................................71

SURA YA SABA ...................................................................91

JINSI YA KUTENGENEZA MSHAHARA WAKO MWENYEWE. NJIA KUMI ZILIZOTHIBITISHWA (HOW TO COMMAND YOUR SALARY) ..........................................................................91

Kujifunza bila kuchoka ..........................................................96

SURA YA NANE ....................................................................106

USISHINDANE KWA BEI LABDA KAMA WEWE NI ROCKEFELLER. VITU SITA AMBAVYO VINAWEZA KUKUFANYA UWE WA KIPEKEE KWENYE SOKO BILA KUPUNGUZA BEI ...106

SURA YA TISA ....................................................................114

KUWAHUDUMIA WATU WENGI ZAIDI ......................114

SURA YA KUMI....................................................................120

KUSIMAMIA KILE UNACHOSEMA ........................................120

SURA YA KUMI NA MOJA...................................................152

VITU VITANO (05) VITAKAVYOKUFANYA UHESHIMIKE .......152

SURA YA KUMI NA MBILI ....................................................159

SABABU 15 KWA NINI HAUPASWI KUWA NA PLAN B .........159

SURA YA KUMI NA TATU ............................................172

KUWA ORIGINAL ...........................................................172

SURA YA KUMI NA NNE ......................................................178

TUNZA MUDA WAKO ..........................................................178

SURA YA KUMI NA TANO...................................................191

KUWA NA VYANZO VINGI VYA KIPATO...............................191

# SURA YA KWANZA

## KUWA NA KITU AMBACHO HAKUNA MTU ANAWEZA KUKIFANYA

Tarehe 15.1.2015, kwenye mtandao wa Quora Kuna mtu aliuliza, nitaweza kuwa bilionea kama nimedhamiria kuwa na nikaweka kazi inayotakiwa? Justin Musk ambaye ni mke wa zamani wa bilionea Elon Musk, alijibu swali hilo kwa kusema HUWEZI. Kwanza kama unataka kuwa bilionea unapaswa kubadili mtazamo kutoka kwenye ubilionea na kuuweka kwenye kitu ambacho watu wanataka. Kisha kuwapa watu huduma katika namna ambayo hakuna kompyuta wala mtu au kitu chochote kile kinaweza kutoa huduma hivyo.

PATA KITABU KIZIMA CHENYE KURASA 200+

GHARAMA YA KITABU NI 20,000/- tu

Na unaweza kukukipata popote pale ulipo duniani.

PATA KITABU KIZIMA CHENYE KURASA 200+

GHARAMA YA KITABU NI 20,000/- tu

Na unaweza kukukipata popote pale ulipo duniani.

## KUHUSU KITABU

Sisi binadamu ni viumbe ambao tunapenda kuthaminiwa, kuheshimiwa na tunataka watu watambue uwepo wetu. Ukienda kwenye mkutano au kwenye sherehe fulani, wakiwatambulisha watu wote halafu wakakuacha wewe bila kukutambulisha, ni wazi utajisikia vibaya na pengine utasema kwamba wamekudharau.

Au ukienda sehemu watu na wote wakapewa vinywaji na chakula, halafu ukasahaulika wewe, ni wazi kuwa wewe mwenyewe utang'aka. Ila upande mwingine wa shilingi, ni kuwa ukienda sehemu watu wakatambua uwepo wako, wakakupa heshima zote. kama ni vinywaji wewe ukapewa kwa kipaumbele, utafahamu kuwa hawa watu wamenithamini, na pengine utataka na wengine wajue hilo.

Thamani ni kitu muhimu sana ambacho unahitaji kuwa nacho.

Kwenye kurasa za kitabu hiki unaenda kujifunza namna ambavyo unaweza kuongeza thamani yako zaidi.

Mbinu unazoenda kujifunza kwenye kitabu hiki zitakusaidia kuongeza thamani yako mara mbili mpaka mara kumi zaidi.

Naomba nieleweke kwamba ninaposema kuongeza thamani yako simaanishi kwamba, utaongeza thamani kwa kuwa mrembo zaidi. Wala simaanishi kwamba utaongeza thamani kwa kupata *followers* zaidi mtandaoni, na wala simaanishi kwamba unaongeza thamani yako kwa kuwa mrefu, mfupi, mtu wa miraba minne, mweusi, mweupe au maji

ya kunde! Endapo hayo yatatokea, basi tutashukuru pia kuwa yametokea.

Bali haswa namaanisha kuongeza thamani yako kwa kulipwa zaidi. Ukitumia mbinu zilizoainishwa kwenye hiki kitabu, ***utakuwa na uwezo wa kulipwa mara mbili mpaka mara kumi zaidi***. Hivi kwa mfano, unaanzaje kuacha kutumia mbinu hizi ili uweze kulipwa zaidi ya unavyolipwa sasa hivi?

## HITIMISHO LA KITABU

Mimi Godius Rweyongeza nimeweka juhudi na kazi kubwa kuhakikisha kwamba unapata kitabu hiki mkononi mwako. Uandishi wa kitabu hiki umenichukua muda kuliko nilivyotegemea mwanzoni.

Ninachotegemea kutoka kwako ni kitu kimoja tu. Kuwa utakisoma hiki kitabu, utakifanyia kazi na utaongeza thamani yako walau mara mbili zaidi ya sasa.

Au kwa lugha rahisi zaidi ni kwamba, nategemea baada ya wewe kuwa umesoma kitabu hiki, uweze kulipwa mara mbili mpaka mara kumi zaidi ya unavyolipwa sasa hivi. Ila utapaswa kufanyia kazi haya uliyosoma kwenye hiki kitabu. Nakutakia utekelezaji mwema wa yale uliyojifunza kwenye hiki kitabu.

Godius Rweyongeza

Disemba 25, 2022 (2:41AM)

Morogoro-Tz

PATA KITABU KIZIMA CHENYE KURASA 200+

GHARAMA YA KITABU NI 20,000/- tu

Na unaweza kukukipata popote pale ulipo duniani.

PATA KITABU KIZIMA CHENYE KURASA 200+

GHARAMA YA KITABU NI 20,000/- tu

Na unaweza kukukipata popote pale ulipo duniani.